ingolewa, alisema

kigeni.

# Tindikali baharini yatishia mazalia ya samaki

Elias Msuya,Mwananchi
emsuya@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Taasisi ya Utafiti wa Samaki (Tafiri) imesema ongezeko la tindikali baharini, linatishia mazalia ya samaki nchini.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi wa Tafiri, Dk Ismael Kimerei alisema kutokana na tishio la ongezeko la tindikali baharini wameweka boya linalopima kemikali hiyo na hali ya hewa ili kutafuta mbinu za kupambana nayo.

"Tindikali ikizidi baharini inasababisha samaki wanaotegemea alkali kuishi kama kambakochi na makombe hufa kwa sababu yale magamba yao yatakuwa dhaifu, uhakika wa uendelevu wao utakuwa mdogo.

Alisema vifaa walivyofunga kwenye boya hilo lililopo baharini ni pamoja na vipima jotoridi la maji na vifaa vya kupimia tindikali. "Pia kwenye boya letu kuna vifaa vya kupimia hali ya hewa na mwelekeo wa upepo kama ni Kusini au Kaskazini na hali ya bahari," alisema Dk Kimerei.

"Pia matumbawe, nyasi bahari na mikoko ndiyo inayoathirika zaidi kwa sababu tindikali ikizidi yenyewe yanayeyuka.

Kwa upande wake, Dk Baraka Sekagende ambaye ni ofisa utafiti wa Tafiri, alisema pia utafiti wao unalenga kupima virutubisho ndani ya majiikiwamo naitrojeni na fosiforasi vinavyoonyesha mwenendo mzima wa uchafuzi wa mazingira baharini. Pia tunaangalia virutubishi maji ambavyo ni chakula cha samaki wadogo. "Tatizo hili linasababishwa na ongezeko la hewa ya ukaa na uchafuzi wa mazingira unaoendelea," alisema Dk Sekagende. Naye mwenyekiti wa ufukwe wa Kunduchi (BMU), Zedi Mwinyi Zedi alisema tangu utafiti huo ulipoanza wamekuwa wakishirikishwa na Tafiri kila hatua. Alitoa wito kwa wavuvi kulinda boya hilo na kuacha kuchomoa vifaa vilivyofungwa.

KUPOTEA KUPOTEA KUPOTEA KWA KUPOTEA KWA KUPOTEA KWA KUPOTEA

Scanned with CamScanner